## MWANZO WA KANISA LETU

Mnamo mwaka wa elfu moja mia saba themanini na saba,Padre. Richard Allen, Padre Absalom



Jones, na kikundi cha wafuasi walijiondoa kutoka kwa Kanisa la Kimethodisti La Mtakatifu George mjini Philadelphia, Pennsylvania kwa sababu ya "maoneo yasiyofaa" na ubaguzi ambao waumini wa ukoo wa Kiafrika walipitia. Walihisi kuwa hawangeweza Kuendelea kuabudu katika mkusanyiko wa kumwabudu Mungu, ambao ulishindwa kuwadhibitisha kama wana (watoto) wa Mungu wenye uwezo na thamani sawa. Kwa sababu hii Allen na wafuasi wake walianza kumwabudu Mungu katika duka la Mfua chuma (Mhunzi). Baadaye,walianzisha kikundi cha Waafrika huru waliojitawala ambacho kilitangulia kabla ya Kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika.

Mnamo mwaka wa elfu moja mia nane na kumi na sita, Richard Allen na wawakilishi kutoka baadhi ya Makanisa ya Kiafrika walikutana, na ushirikiano wa Kanisa ama "Muungano" ukatengenezwa uwe kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika.

Richard Allen alikuwa mwanzilishi na Askofu wa kwanza kuchaguliwa na kuwekwa wakfu (kubarikiwa). Walianzisha dhehebu la kwanza la Waafrika Wamarekani; liliruhusu na bado linaendelea kuruhusu watu wenye asili ya Kiafrika uwezo wa kujiheshimu,adhama na Uhuru wa kumwabudu Mungu kabisa, na kushiriki kwa kiwango chenye ukamilifu katika kujenga ufalme wa Mungu.

## UJUMBE WETU

Ujumbe wa Kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika ni kuhudumia ukuaji wa watu wote Kijamii, Kiroho na Kimwili.

## MAELEZO YA JINA LA KANISA

**Afrika** – Inamaanisha kuwa Kanisa lilipangwa na watu wenye asili na urithi wa Kiafrika. Hili halimaanishi kuwa Kanisa lilipangwa na kuanzishwa katika eneo la Afrika ama ni Kanisa la watu wenye asili ya Kiafrika pekee. Hili linamaanisha kuwa Wamarekani walioanzisha walikuwa wenye asili ya Kiafrika, na kwa hakika tunajivunia kutambua jambo hili.

**Methodisti** – Inarejelea wafuasi wa Kanisa katika jamii ya Kanisa za Kimethodisti. Richard Allen, mwanzilishi na Askofu wa kwanza mwenye bidii, alihisi kwamba mafundisho ya dini na taratibu za Kimethodisti zingefaa zaidi kwa mahitaji ya jamii ya Kiafrika.

**Askofu** – Inarejelea hali ya utawala ambao Kanisa huendeshwa. Utawala huu wa Kiaskofu humaanisha kuwa Maafisa wakuu wa dhehebu hili ni Maaskofu. Mamlaka yao wamepewa na kikundi cha mkutano mkuu, jinsi walivyochaguliwa ili kusimamia shughuli za kanisa; pamoja na kuongoza mikutano ya kila mwaka, kuteua watu kwa kazi ya ukasisi, kuteua mashemasi na wazee wa kanisa, kupanga shughuli za utume na kwa ujumla kuchangia katika kuinua shughuli za dhehebu.

**Kanisa** – Inarejelea "kanisa la Kikristo" ambalo ni muungano wa watu ambao wanamwamini Mungu na ambao wamemkubali Yesu Kristo kama mfano bora wa kuyaongoza maisha yao. Bado tunaamini katika kiumbe wa watu ndani ya Mungu baba, Roho Mtakatifu, ambaye humwezesha mwenye imani kuwa mfuasi mkweli na mfaafu wa Mungu.Yesu Kristo ndiye kiongozi wa kiroho katika Kanisa la Kikristo.

## WITO WETU

Wito wa Kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika ni Mungu Baba Yetu, Kristo mkombozi wetu, Roho Mtakatifu mfariji wetu, Wanadamu familia yetu.

## IMANI ZETU

Katika mafundisho yetu yaliyotokea zamani,kuna baadhi ya maandiko ambayo husaidia kujulisha njia zetu za kipekee za kuelewa imani ya Kikristo. Tunategemea: Kitabu cha mafundisho ya Dini na nidhamu ya Kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika, Kitabu cha nyimbo za dini cha kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika, Kitabu cha ibada cha kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika, Maamkizi ya Maaskofu, Masimulizi ya kihistoria, Nakala za dini na Injili za Utumishi wa Padre Mstaafu. Richard Allen.

Kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika linatambua na kuchunguza sakramenti mbili takatifu: Ubatizo na ushirika Mtakatifu

Njia za ubatizo katika mafundisho ya jamii ya Wakristo wa Kimethodisti ni kumwagilia, kunyunyuzia na kutumbukiza.Bila kujali njia ambayo itatumiwa, ubatizo ni ishara yenye nguvu ya uzazi wa pili (kwa jinsi ya roho) na kuingizwa katika jamii ya watu wanaokaa pamoja kwa imani-kanisa la kristo.

Ushirika Mtakatifu hutumiwa kama ukumbusho wa kifo na mateso ya Kristo na kusherehekea wingi wa uzima tulionao kupitia kwake.

## UTAWALA WETU

Kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika lina mikutano tano: ❖ Mkutano wa wafuasi wote kwa jumla ❖ Mkutano wa kila mwaka ❖ Mkutano wa wilaya ❖ Mkutano wa baada ya miezi mitatu ❖ Mkutano wa kanisa

**Mkutano Wa Wafuasi Wote (Watu Wote):** Hiki ndicho kiwango cha juu sana kinachounda sheria katika kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika. Hukutana baada ya miaka minne kuchagua Maaskofu na maafisa wakuu na kufanya sheria. Baraza la Maaskofu ndilo kundi lenye kuangalia makosa ya kiutawala na kutoa mwongozo katika dhehebu.

Baraza la korti ndilo hutoa hukumu ambayo hutatua lawama za mwisho katika mambo ya sheria zilizowekwa waziwazi.

**Mkutano Wa Kila Mwaka:** Huu ndio msingi katika kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika ambao hukutana kila mwaka ili kuangalia ripoti za wazee watawala, makasisi na wanakamati. Askofu ndiye afisa mkuu anayeongoza mkutano huu. Ndani yake kuna mapadre na mtu mmoja wa kawaida aliyetumwa kuwakilisha kila moja ya kanisa katika mahali pamoja.

**Mkutano Wa Wilaya:** Huu ni mkusanyiko wa kanisa zilizoko katika wilaya yenye uongozi mzee ambayo hukutana kila mwaka kuchunguza kazi ya miungano midogo,na kukagua watu wanaotaka kupata cheo cha kufanywa padre na kuzingatia kazi kwa manufaa ya kanisa zote. Kiongozi mzee ndiye afisa mkuu anayeleta muungano kati ya kanisa zilizoko katika eneo moja na ile kubwa yenye kuleta mwunganisho.

**Mkutano Wa Baada Ya Miezi Mitatu:** Huu ndio mwungano unaotawala kanisa zilizoko katika eneo moja ambapo mipango, sera na utendakazi huangaliwa na kukadiriwa. Kiongozi mzee ndiye Kiongozi mkuu anayeleta muungano kati ya kanisa zilizoko katika eneo moja na ile kubwa yenye kuleta muungano.

**Mkutano Wa Kanisa:** Huhusu kanisa zilizoko mahali pamoja na hukutana ili kujadili kazi ya kanisa kwa ujumla na kuzingatia jambo la upekee ama mradi. Kasisi ndiye Kiongozi mkuu.

## UONGOZI WETU

Maaskofu,viongozi wazee na mapadre hutawala na kuelekeza idara za kiroho na idara za muda za kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika katika vitengo mbalimbali vya mikutano ya kanisa.

Maaskofu huchaguliwa na kuwekwa wakfu (kubarikiwa) kwa kazi ya uaskofu na huhudumu kwa makanisa yaliyo enea kote ulimwenguni. Kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika huweza kupatikana katika zaidi ya nchi arobaini.Viongozi wazee waliochaguliwa na Kiongozi Askofu huhudumu kama watawala na washauri waunganishi kati ya mkutano wa kila mwaka na kanisa lililoko mahali maalum katika kiwango cha mtaa. Wao huhakikisha kuwa makanisa ya mitaani na huduma zao zinafanya kazi vizuri na zinalingana na mashauri na utaratibu wa kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika.

Mapadre walioteuliwa na Kiongozi Askofu huhudumu kama maafisa wakuu wa muungano wa mitaani na wana jukumu la kuhakikisha mambo yote yametendwa jinsi ilivyokusudiwa. Wao huchagua watumishi wasaidizi wa kanisa za mitaani ambao hudhibitishwa na mkutano wa baada ya miezi mitatu na huhudumu kama kitengo cha utawala.

Makasisi hutaja wadhamini ambao huchaguliwa na kanisa za mitaani na husimamia na kuangalia jinsi kanisa za mitaani zinavyokuwa.

*Mafundisho ya dini na nidhamu ya kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika* hutumika kama katiba ya kanisa la kikristo na kuonyesha nakala za dini, sheria za kijumla, kanuni za dini na shughuli zingine za kanisa.

## SURA YETU

Kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika linajumuisha yafuatayo: ❖ Wafuasi milioni mbili na elfu mia tano ❖ Mapadre elfu nane ❖ Mikusanyiko ya waumini elfu sita na mia mbili ❖ Wilaya ishirini zinazoongozwa na Maaskofu ❖ Mikutano mia moja kumi na tano kila mwaka

## IDARA ZETU, TUME, MASHIRIKA NA UCHAPISHAJI

Kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika lina idara na tume zifuatazo za kushughulikia mahitaji katika maisha ya kanisa.

**Idara:** ❖ Elimu ya kikristu ❖ Ukuaji na kuendelea kwa kanisa ❖ Mashahidi duniani na kazi ya Upadre ❖ Fedha zilipwazo kila mwaka ❖ Fedha za kupata faida na bima ❖ Mwandishi wa mambo ya Kikristo ❖ Mambo ya Fedha ❖ Ofisi ya katibu mkuu ❖ Utafiti na fedha za kuendelea katika mafundisho ❖ Muungano wa kufundisha watoto jumapili,elimu ya dini ya kikristo ya kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika.

Idara za kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika huhudumia orodha ya mambo ya umoja wa jamii ya watu na majukumu ya kanisa.

Kazi ya kila idara inaongozwa na afisa mkuu ambaye huchaguliwa na watu katika mkutano mkuu.

**Tume:** ❖ Takwimu na Fedha ❖ Fedha zilipwazo kila mwaka za kupata faida na Bima ❖ Uchapishaji ❖ Matendo ya kikundi ❖ Kukua na kuendelea kwa kanisa ❖ Mashahidi wa kimataifa na kazi ya upadre ❖ Seminari za watu wasio Mapadre na wasio na elimu maalum ❖ Vyuo ❖ Shule na vyuo vikuu ❖ Elimu ya kikristo ❖ Wanawake katika huduma ❖ Idara ya Afya na ajira ❖ Maendeleo ya kimataifa ❖ Maendeleo ya kiuchumi ❖ Wachungaji

**Mashirika:** Vikundi vya wanawake wamishenari ❖ Muungano wa watu wa kawaida ❖ Kitengo cha watu wenye umri mdogo ❖ Kikundi cha watu wa umri wa Kati cha Richard Allen ❖ Wajumbe wa muziki na Sanaa ya Kikristo ❖ Wanawake katika huduma ❖ Ushirika wa wataalamu wa kanisa ❖ Muungano wa wanaskauti wa kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika ❖ Wahudumu Waunganishi ❖ Wanandoa ❖ Muungano wa Wajane pamoja na P.K.s ❖ Baraza unganishi ❖ Wana wa kiume wa Allen ❖ Baraza la Wazee viongozi ❖ Debutante ya Kikristo_Tume ya Mabwana

**Machapisho:** ❖ Ukaguzi wa kanisa la Kimethodisti la Kiaskofu la Kiafrika ❖ Mwandishi wa Kikristo ❖ Kitabu cha mambo ya kila siku cha elimu ya Kikristo ❖ Jarida la wanawake wamishenari ❖ Sauti ya utume ❖ Barua ya kujuza habari za mambo yaliyotokea karibuni ya Y.P.D.

*Tafsiri na Mchungaji Dkt.Wilson Mugambi Arimi, Bi Trizia Wangari, Bwana Kenneth Kimathi, Mheshimiwa Mark Mawira Alberto*

### HII NI RASILIMALI INAYOWEZA KUPAKULIWA BURE ILIYOTOLEWA NA:


Idara ya Elimu ya Kikristo
P. O. Box 331947
Nashville, TN 37203
Ph: (615) 242-1420
Fax: (615) 726-1866
cedoffice@ameced.com
www.ameced.com


**KANISA LA KIMETHODISTI LA KIASKOFU LA KIAFRIKA**

# WATU WA FUAWE

*Kanisa La Kimethodisti La Kiasofu La Kiafrika lilianza kwa malalamiko, likazaliwa kwa maombi katika madhabahu, na likapewa umbo la fuawe ya Mungu katika duka la mfua vyuma.*

***Sisi Ni Watu Wa Fuawe.***